BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tisa – Tarehe 27 Februari, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

141. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa vijana wa Fumba, Bweleo, Nyamanzi na maeneo mengine wamejiajiri katika sekta ya utalii kwa kusafirisha watalii wanaokuja na kuwapeleka kisiwa cha Kwale. Na kwa kuwa kwa muda mrefu sasa usafirishaji huo umekuwa ni ajira kwa vijana hao na wanaitegemea kwa kuwapatia riziki na familia zao. Na kwa kuwa Serikali kwa nia njema imeamua kukikodisha kisiwa hicho kwa wawekezaji.

(a) Je, vijana hao waliojiajiri wataendelea kufanya kazi za kupeleka watalii katika kisiwa hicho ama hawataruhusiwa tena.

(b) Kama hawataruhusiwa tena, je Serikali ina mpango gani mbadala wa kuwasaidia ili wasipoteze ajira zao na kurudisha nyuma maisha yao.

(c) Baada ya kukodishwa kisiwa cha Kwale, je ni upi mustakbali wa wavuvi wanaotumia maeneo ya kisiwa hicho katika shughuli zao za uvuvi.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

148. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Eneo la Maduka ya Biashara kuanzia Mlandege kupitia Mchangani mpaka Darajani ni maarufu kwa shughuli za biashara kuanzia asubuhi mpaka jioni na katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani shughuli zinafanyika mpaka usiku, na kunakuwa na msongamano mkubwa wa watu wakijipatia mahitaji mbali mbali. Hata hivyo, kumekuwa na adha ya vyombo vya moto kama gari, piki piki, bajaji na mikokoteni kutumia njia ya madukani na kusababisha kero na hali hatarishi kwa wananchi.

(a) Kwanini Serikali kupitia Baraza la Manisipaa Mjini isiweke kizuwizi cha matumizi ya vyombo vya moto kuanzia Mlandege, kupitia Mchangani mpaka Darajani kuanzia wakati wa asubuhi mpaka jioni, ili kuondoa kero hiyo.

(b) Kwanini Baraza la Manispaa lisiweke utaratibu kwa wale wafanyabiashara wanaoleta mizigo yao madukani wautumie wakati wa usiku ambao shughuli za biashara zinakuwa zimemaliza.

(c) Je, Baraza la Manispaa lipo tayari kuweka mpango usioleta adha na kero ya matumizi ya vyombo vya moto katika eneo la madukani kutoka Mlandege mpaka Darajani.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

54. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni ukweli ulio dhahiri kwamba Utamaduni wa Mzanzibari unaendelea kuporomoka na kupelekea kupotea kwa tunu na vionjo vinavyomtambulisha Mzanzibari. Mila, silka na desturi za watu wa Zanzibar ambazo zimekuwa ni mojawapo ya vivutio vikubwa kwa wageni wanaofika na kutembelea nchi yetu, zimeachwa bila ya kuwa na mpango maalum wa kuzitunza na kuzirithisha kwa vizazi vijavyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani bora wa muda mfupi na

muda mrefu wa kuhakikisha inalinda mila, desturi na silka za Mzanzibari, ili kusaidia kulinda utamaduni wetu na kupunguza tatizo la kuporomoka kwa maadili.

(c) Je, kwa miaka mitano iliyopita, Serikali imetekeleza mpango gani wa kawaida na wa maendeleo wa kuuhuisha na kuuhifadhi utamaduni wa Mzanzibari.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

171. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kisiwani Pemba, kuna wananchi ambao nyumba zao ziliathirika katika zoezi hilo. Katika tathmini iliyofanywa, wako ambao walipata fedha kidogo sana na hawakuzipokea fomu za malipo na kuzirudisha ZURA.

Je, Serikali imechukua hatua gani kumaliza kadhia hiyo.

**Wizara ya Afya:**

72. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na huduma nzuri zinazotolewa katika hospitali zetu za Zanzibar bado kumekuwa na changamoto nyingi zinazojitokeza kila siku katika suala zima la vifaa tiba, ambavyo vingesaidia kuchunguza magonjwa mbali mbali kwa wananchi wanaohitaji huduma hiyo ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri huoni sasa ipo haja ya kutafuta vifaa tiba vya kisasa ili kuepukana na kufanya kazi kwa mazoea.

(b) Je, ni muda gani sasa wananchi wamekosa kufanyiwa vipimo vya afya zao hasa maradhi ya tezi dume.

(c) Je, Wizara inalibeba vipi tatizo hili na kuhakikisha kuwa hivi sasa wananchi hawapati usumbufu wa huduma hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

34. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa maonesho ya siku ya chakula duniani yaliyofanyika Chamanangwe kisiwani Pemba yameibuwa hisia za wakaazi wa Pemba hususan katika maeneo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa njia za kitaalamu, sambamba na taaluma ya kupunguza uharibifu wa misitu kwa kutumia majiko pamoja na nishati mbadala. Na kwa kuwa maonesho pamoja na taaluma inayotolewa ni ya muda mfupi na haikidhi ufahamu wa wakulima pamoja na wajasiriamali walio wengi.

    Je, ni lini Wizara yako kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, itaanzisha Kitivo cha Kilimo na Ujasiriamali (Faculty of Agriculture and Entrepreneurship), Tawi la Pemba (Pemba Branch), ili mafunzo hayo yawe endelevu.

113. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Miongoni mwa skuli zenye upungufu wa walimu ni pamoja na skuli ya Makongeni Mtambwe ambayo ina walimu wawili tu wanaolazimika kufundisha madarasa kuanzia darasa la 9 hadi darasa la 12.

    Je, ni lini skuli hiyo itapatiwa walimu kulingana na idadi ya madarasa na wanafunzi waliopo sasa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

115. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Shehia ya Mbweni na Chukwani hazipati huduma ya maji safi na salama kwa zaidi ya mwaka na miezi kadhaa na ukizingatia kuwa Mhe. Waziri uliwahi kutoa ahadi kuwa Wizara yako itaitatua changamoto hiyo ndani ya wiki mbili, ingawaje ahadi hiyo bado haijatekelezwa hadi leo.

    Je, ni kikwazo gani kilichopelekea hadi leo hii kadhia hiyo kutopatiwa ufumbuzi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

80. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na uzururaji ovyo na wizi mkubwa bandarini hususan wakati meli kutoka Pemba zinapofunga nanga Bandarini Unguja.

Je, Serikali imejipanga vipi kutokana na kadhia hii.

100. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Mhe. Waziri tumekusikia kupitia vyombo vya habari kikiwemo cha ZBC ukiwaeleza wakandarasi wanaojenga barabara ya njia kongwe Chake-Wete, kuwa barabara hiyo inajengwa kwa mwendo wa kusuasua na kutoridhishwa na utendaji wao wa kazi.

(a) Je, ni asilimia ngapi ya ujenzi huo imefikiwa mpaka sasa.

(b) Ni changamoto zipi ambazo umeziona katika ujenzi huo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

61. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Miongoni mwa neema tulizonazo hapa visiwani ni kuwa na mabonde mbali mbali yanayoweza kutumiwa kwa kilimo cha mpunga na kilimo chengine kinachofanana, iwapo wananchi wetu watawezeshwa ipasavyo kuyatumia mabonde hayo.

(a) Ni lini Wizara itatekeleza kwa vitendo azma njema ya Serikali yetu ya kuyatumia mabonde ya mpunga kama vile Cheju, ili kuweza kujitosheleza kwa uzalishaji wa mchele wetu wenyewe.

(b) Je, kuna changamoto zipi zinazopelekea kukwama kwa kipindi kirefu, azma hiyo njema ya Serikali.

(c)

62. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali yetu ya kuwawezesha wakulima, kwa muda mrefu sasa, wakulima wetu wadogo wadogo hapa Zanzibar, wamejikita zaidi katika uzalishaji wa kilimo cha kujikimu, badala ya sasa kujishughulisha na kilimo cha biashara.

Je, Wizara yako imefanikiwa vipi kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kutoka katika uzalishaji wa kilimo cha kujikimu kwenda katika kilimo cha biashara.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

30. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Makumbusho ni sehemu muhimu sana inayohifadhi na kutunza alama na vielelezo mbali mbali vya historia ya nchi yetu.

(a) Je, tuna aina ngapi za makumbusho ya watu binafsi yaliyosajiliwa rasmi Zanzibar.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuyasajili makumbusho hayo.

(c) Je, makumbusho hayo yana mchango gani katika kukuza pato la Taifa nchini kwetu.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**27 Februari, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**